**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 21 Septemba, 2018.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2017/2018.

**Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2017/2018.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2017/2018.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2017/2018.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:**

88. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Kumekuwa na tabia inayokera kwa Idara ya Uhamiaji upande wa Zanzibar kutokitambua kitambulisho cha Mzanzibari kama nyaraka ya kuombea hati ya kusafiria.

Kwa kuwa wakaazi wa Zanzibar wanakitumia kitambulisho hicho kwa shughuli mbali mbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Na kwa kuwa Idara ya Uhamiaji inahudumia wananchi wa Tanzania waliopo Zanzibar.

(a) Je, kukataa kukitambua kitambulisho hicho cha Mzanzibari si kudharau nyaraka halali ya kisheria na kuwakosesha Wazanzibar haki zao.

(b) Je, kitendo cha Idara ya Uhamiaji si sawa na kudharau Mamlaka ya Rais wa Zanzibar ambaye amesaini Sheria ya kutumika kitambulisho hicho.

(c) Je, SMZ itachukua hatua gani kuhakikisha Idara ya Uhamiaji inakitambua kitambulisho hicho ambacho kinatumika hata kumpa haki Mzanzibari kupiga kura ya kuchagua viongozi wa Zanzibar na Watanzania.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

111. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Barabara ya Masingini Chake ilipangiwa kufanyiwa matengenezo katika bajeti ya mwaka 2017/2018. Hata hivyo, barabara hiyo mpaka hivi sasa haijafanyiwa matengenezo.

(a) Je, ni sababu gani zilizosababisha kutokuanza kwa matengenezo ya barabara hiyo mpaka hivi sasa.

(b) Je, ni lini inategemewa kuanza matengenezo ya barabara hiyo.

(c) Je, inategemewa kuchukua muda gani kwa matengenezo ya barabara hiyo mpaka kumalizika.

112. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Pamoja na jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuimarisha miundombinu ya biashara, bado kijiji kipya kinachotoka Michakaini kuendea Pagali kupitia Ngomahazingwa katika Jimbo la Chake Chake kina ukosefu wa barabara kwa kiwango cha lami au kifusi.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara kutoka Michakaini kwenda Pagali kupitia Ngomahazingwa ambapo itakutana na barabara inayotoka Gombani Mwembe Karata kuelekea Pondeani Wesha.

(b) Kama Serikali ina mpango wa kujenga barabara hiyo, Je, itajengwa kwa bajeti ya mwaka gani.

(c) Je, barabara hiyo imeshapimwa.

**Wizara ya Biashara na Viwanda**

56. MHESHIMIWA SHEHE HAMAD MATTAR (Jimbo la Mgogoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika awamu zilizopita iliwahi kufanya majaribio ya kuwa na kiwanda cha saruji hapa Zanzibar.

(a) Je, majaribio yale yalileta matokeo gani.

(b) Kama utafiti huo ulionesha mafanikio, kwa nini sasa hatukuendeleza kiwanda hicho.

c) Kama utafiti huo haukukamilika, kwa nini hatukuendeleza utafiti huo ili kusaidia uchumi wa Zanzibar.

**Wizara ya Elimu Na Mafunzo ya Amali:**

3. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika kipindi cha miaka michache iliyopita, Serikali ilipiga marufuku masomo ya ziada nyakati za usiku (tuition) kwa sababu hazina udhibiti na zinapotosha wanafunzi. Hivi karibuni wimbi kubwa la masomo ya ziada limeibuka lakini zaidi kumeibuka na kambi za masomo zinazoendeshwa na watu binafsi bila ya udhibiti wa Wizara.

(a) Je, kuibuka kwa kasi kubwa masomo ya ziada ya usiku, inamaanisha kuwa wanafunzi wetu hawasomeshwi maskulini.

(b) Je, kuwepo kwa kambi za mitihani, Wizara imetoa ruhusa ya kambi hizo hasa zile zinazoendeshwa na watu binafsi majumbani mwao.

(c) Je, kuna utaratibu wowote wa ufuatiliaji wa masomo ya ziada ya usiku na kambi za mitihani kama zinafanyika katika vigezo vinavyokubaliwa na Wizara.

**Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:**

45. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) **-** Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Zanzibar ni nchi ya visiwa ambavyo vimezungukwa na bahari ambayo ina samaki wengi, lakini hivi sasa Zanzibar inaletewa samaki kutoka nchi za nje yaani peduu.

(a) Je, Wizara inalijua hili.

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa kuwaendeleza wavuvi ili kuvua samaki wa kutosha.

**Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale:**

71. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

Utalii ni sekta muhimu kwa uchumi wa nchi pamoja na ajira kwa wananchi. Hata hivyo, wageni wengi hufanya kazi ambazo wazawa wanaweza kuzifanya yaani kuendesha biashara ya usafiri wa wageni kama taxi, gari za abiria (private hire), boti za watalii, nk. na hivyo wazawa kukosa fursa hizo za kujiajiri.

Je, Serikali haioni haja ya kuweka mkakati maalumu kama sheria ya utalii inavyoelekeza kuwa kazi ambazo zinaweza kufanywa na wazawa zisifanywe na wageni.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:**

33. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Ujenzi wa Bandari ya Wete ambayo kwa wafanyabiashara kati ya Pemba na Tanga unazungumzwa kwa muda mrefu. Hata hivyo, ujenzi huo bado haujaanza jambo ambalo ni kilio cha muda mrefu cha wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, ambao hulazimika kutumia majahazi na kusababisha ajali nyingi na watu kadhaa kupoteza maisha.

(a) Je, hadi sasa suala la ujenzi wa Bandari ya Wete umefikia wapi, sambamba na kupatikana chombo cha dharura cha uhakika ambacho kitatumika kwa ajili ya usafiri kati ya Bandari ya Wete na Tanga.

(b) Je, mazungumzo kati ya Serikali na Kampuni ya Azam Marine kwa ajili ya ujenzi wa Bandari hiyo yamefikia wapi na upi mwelekeo wa Kampuni ya Azam Marine kuhusu ujenzi huo.

(c) Je, Shirika la Meli halioni kwamba kwa sasa ipo haja ya kutafuta meli ndogo japo ya kukodi ambayo itatoa huduma ya usafiri wa abiria kati ya Bandari ya Wete na Tanga ili kuwapunguzia tatizo la usafiri wa abiria na mizigo.

**III. HOJA ZA SERIKALI:**

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:**

Ripoti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2017/2018.

**Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:**

Ripoti ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2017/2018.

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**21 Septemba, 2018.** **KATIBU WA BARAZA.**